



RASIMU YA TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

BENKI KUU YA TANZANIA YATOA GAWIO LA SH. BILIONI 300 KWA SERIKALI

Bodi ya Wakurugenzi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeidhinisha gawio la sh. bilioni 300 kwa Serikali kutokana na faida iliyoapatikana kwa mwaka wa fedha wa 2016/17.

Kifungu cha 18 (5) cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006 kinaipa Benki Kuu mamlaka ya kutoa gawio kwa Serikali pale inapotengeneza faida.

Majukumu ya msingi ya Benki Kuu sio kutengeneza faida; hata hivyo, inapotokea kwamba faida imepatikana, sehemu kubwa hutolewa kama gawio kwa Serikali.

Kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006, jukumu la msingi la Benki Kuu ya Tanzania ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha inayolenga kudhibiti mfumuko wa bei na kujenga mfumo wa fedha ulio imara na unaofaa kwa ukuaji endelevu wa uchumi wa taifa.

Majukumu mengine ni kuchapisha noti na sarafu za Shilingi ya Tanzania; usimamizi wa mabenki na taasisi za fedha; kusimamia na kudhibiti mifumo ya malipo ya taifa; kuhifadhi akiba ya fedha za kigeni ya taifa; kutoa ushauri wa kiuchumi na fedha kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; ni Benki ya Serikali hizo na taasisi zake, na ni benki ya Mabenki.

Prof. Benno Ndulu
Gavana
Benki Kuu ya Tanzania
Desemba 28, 2017

governoroffice@bot.go.tz